

Mwaka mmoja baada ya kifo cha Samora

LEO umetimia mwaka mmoja tangu Rais Samora Machel wa Msumbiji afariki katika ajali ya ndege ambayo mpaka hapo itakapothibitishwa vinginevyo, dunia nzima inaamini kwamba ilisababishwa na hujuma za Makaburu. Katika makala hii, JOHN MORRISON wa *Reuters* anaeleza hali ilivyo nchini humo mwaka mmoja baada ya kifo cha mwanamapinduzi huyo.

MWAKA mmoja baada ya kumpoteza Rais wake wa kwanza hayati Samora Machel katika ajali ya ndege ambayo watu wengi duniani wanapenda kuamini kuwa ilisababishwa na utawala wa Makaburu, Msumbiji bado inakabiliwa na matatizo makubwa ya uchumi yanayozaliswa hasa na vitendo vya hujuma vinavyofanywa na magaidi wa Renamo.

"Mwaka mmoja uliopita, Msumbiji haikuwa na mahali pengine kwa kwenda bali kusonga mbele kijasiri", anasema balozi mmoja wa nchi ya nje akikumbuka Oktoba 19 mwaka jana wakati ndege ya hayati Samora ilipogonga mlina na kuanguka baada ya kutoka katika njia yake na kuingia Afrika Kusini ikiwa inatokea Zambia katika mazingira ambayo yanaonyesha kila dalili ya hujuma za Makaburu.

Kwa nchi ambayo uchumi wake ulikuwa umeanguka, inakabiliwa na vita dhidi ya magaidi wanaoungwa mkono na Makaburu na inapambana ana kwa ana na ukame, kupoteza Rais wa Chama na Serikali lilikuwa ni pigo lisilomithilika.

Miezi 12 baadaye, wasiwasi uliokuwepo kwamba Serikali ya FRELIMO ingeanguka au kwamba asingepatikana kiongozi

jasiri kama Samora wa kuiongoza nchi, hiyo inayokabiliwa na mafatizo mengi na makubwa umedhihirika wazi kuwa haukuwa na msingi.

Joaquim Chissano, Waziri wa Mambo ya Nje wa Msumbiji tangu ipate uhuru ambaye alichaguliwa kuchukua nafasi ya Samora amedhihirisha kuwa kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi.

Ndugu Chissano amechukua hatua kadhaa za kufufua na kuimarisha uchumi ambazo zilitungwa hata kabla ya Rais Samora kufariki na ametumia ujuzi wake katika medani ya diplomasia kuimarisha uhusiano wa Msumbiji na nchi za nje.

Bado hali ni mbaya mjini Maputo na mikoani hasa vijijini ambako magaidi wa Renamo wanafanya kila kitendo cha hujuma dhidi ya juhudi za kufufua uchumi, kama vile kubomoa madaraja, kuchoma moto mazao nakuua wananchi wasio na hatia.

Kikundi cha Renamo ni cha kinyama na kikatili kiasi kwamba hata Rais Reagan wa Marekani ambaye ana kawaida ya kuvikumbatia vikundi vya kiuaji na kimumiani kama vile UNITA, Contra na Mujaheddin ameshindwa mpaka sasa kukiunga mkono waziwazi kikundi hicho cha Renamo ambacho kimedhihi-



HAYATI Samora akitoa heshima bendera ya Msumbiji ilipokuwa inapandiswa siku ya uhuru.

risha kwa vitendo kwamba kimejawabwa kiu kubwa ya damu ya wananchi wa Msumbiji.

Baada ya uhuru mwaka 1975, Wareno karibu wote waliondoka nchini Msumbiji. Kwa sababu hata makondakta wa mabasi walikuwa Wareno, hakuna wazalendo wa kutostia ambao walikuwa na elimu, ujuzi nauzoefu wa kuanzisha mambo. Hicho ndicho chanzo kikuu cha kuzorota kwa uchumi na huduma mara baada ya uhuru, hali ambayo ilichangiwa

sana na vita vya hujuma na ukame.

Hata hivyo baada ya nchi hiyo kulegeza masharti ya uchumi na kufiki amakubaliano na Shirika la Fedha Duniani (IMF), maduka yameanza kujaa bidhaa ingawa bei zake hazilingani kabisa na mapato ya wananchi walio wengi. Fedha ya nchi hiyo imeshushwa thamani kutoka Meticais 40 kwa dola moja kwa dola moja. Marekani hadi Meticais 400 kwa dola moja.

Hata hivyo masharti hayo ya IMF yameleta matatizo makubwa

kwa wananchi kwa sababu bei za vitu zimepanda sana wakati mapato yanashuka. Mmoja wa Mataifa unakadiri kuwa hivi sasa wastani wa mapato yaliyotupia Msumbiji ni kati ya dola 100 na 140 kwa mwaka ikiwa yalishwa na dola 230 mwaka 1987. Takwimu hizo zinaifanya Msumbiji kuwa moja ya nchi fukara kwa dunia.

Ingawaje Juni mwaka huu Msumbiji ilikuwa ina wakopeshaji wake wahirishitarehe ya kuanza kufika madaraka kwa muda wa miaka 20 gogo, bado nchi hiyo itaendelea kuhitaji misaada mingi ya fedha na chakula kwa muda mrefu ujao.

Wataalamu wa Benki ya Dunia na IMF wamekadiri kuwa pato la taifa la Msumbiji lilikuwa likididimia kwa asilimia 12.8 kati ya mwaka 1982 na 1985. Mwaka 1986, pato hilo lilikuwa kwa asilimia 0.5 tu. Mapato ya fedha za kigeni yalishuka kutoka dola milioni 229 mwaka 1982 hadi dola milioni 79 mwaka jana. Mapato hayo ya fedha za kigeni yanatarajiwa chini ya mipango wa kufufua uchumi kuuwa hadi dola milioni 156.3 mwaka 1990.

Hata hivyo, mapato hayo ya 1990 yatakuwa ni asilimia 18 tu ya nakisi ya malipo iliyoko hivi sasa na asilimia 19 tu ya gharama za uagizaji bidhaa kutoka nje. Kwa sababu viwango vya ulipaji wa riba vitapanda kutoka dola milioni 177 za mwaka jana hadi zaidi ya dola milioni 200 ifikapo mwaka 1990, Benki ya Dunia na IMF wanakadiri kuwa Msumbiji itahitaji kupata dola bilioni 1.1 kutoka nje kila mwaka kati ya sasa na 1990.

Salmao Mambo, Mkuu wa Shirika la Misaada kwa waliopatwa na maafa la Msumbiji anasema: "Siyo nia yetu kuishi kwa misaada. Tunao uwezo wa kujilisha na kuuzza ziada, lakini ili tuweze kufanya hivyo, tunahitaji amani."